



GRETCHEN WHITMER
GOVERNOR

STATE OF MICHIGAN
OFFICE OF THE GOVERNOR
LANSING

GARLIN GILCHRIST II
LT. GOVERNOR

AMRI YA UTENDAJI

No. 2020-37

Kuzuiwa kwa muda kwa kuingia hospitalini, nyumbani kwa wagonjwa, makazi ya pamoja ya wagonjwa, na magereza ya watoto

Mabadiliko ya Amri ya Utendaji 2020-7

Kirusi kipya cha korona (COVID-19) ni ugonjwa unaohusiana na upumuaji na unaweza kusababisha kuugua vibaya au kifo. Ugonjwa huu unaletwa na aina mpya ya kirusi cha korona ambacho hapo awali hakikuhusiana na binadamu na kinachoambukiza kutoka mtu mmoja hadi mwingine. Hatari ya kuugua vibaya au kufa kutokana na kirusi cha COVID-19 hutokea hasa miongoni mwa wazee na watu wenye maradhi sugu. Pia, kuna kuongezeka kwa hatari ya maambukizi ya kirusi cha COVID-19 miongoni mwa watu ambao wanaishi katika mahali penye watu wengi, kama vile, makazi ya wagonjwa. Hadi sasa, hakuna chanjo iliyoidhinishwa au matibabu ya kuzuia na kutibu ugonjwa huu.

Tarehe 10, mwezi wa tatu, mwaka wa 2020, Idara ya Afya na Huduma za Watu ya jimbo la Michigan iligundua kuwepo kwa visa viwili vya kirusi cha COVID-19 katika jimbo la Michigan. Siku hiyo hiyo, nilitoa Amri ya Utendaji 2020-4. Amri hii ilitangaza hali ya dharura katika jimbo lote la Michigan chini ya sehemu ya 1 ya kifungu cha 5 cha sheria ya Katiba ya Michigan ya 1963, Sheria ya Usimamizi wa Dharura, 1976 PA 390, ilivyofanyiwa marekebisha, MCL 30.401-.421, na Sheria ya 1945 PA 302 ya Mamlaka ya Dharura ya Gavana, ilivyobadilishwa, MCL 10.31-.33.

Katika wiki tatu zilizofuata, kirusi hicho kilienea katika jimbo la Michigan, kusababisha vifo vya mamia ya watu, visa vya watu waliothibitishwa kuwa na ugonjwa huo kufikia maelfu, na kuvuruga uchumi wa jimbo hili, makazi, na taasisi za kielimu, za watu wote, kijamii, na kidini. Kuitikia madhara makubwa ya kiafya, kiuchumi, na kijamii yaliyoletwa na ugonjwa wa Korona, nilitoa Amri ya Utendaji 2020-4 na kutangaza hali ya dharura na hali ya jangwa katika jimbo lote la Michigan chini ya sehemu 1 ya kifungu cha 5 cha Katiba ya Michigan ya 1963, na Sheria ya Usimamizi wa Dharura, na Sheria ya Mamlaka ya Dharura ya Gavana ya 1945.

GEORGE W. ROMNEY BUILDING • 111 SOUTH CAPITOL AVENUE • LANSING, MICHIGAN 48909
www.michigan.gov
PRINTED IN-HOUSE

Sheria ya usimamizi wa dharura inampa gavana mamlaka mapana na majukumu “kukabiliiana na hatari zinazotisha jimbo hili au wakazi wa jimbo hili kutokana na janga au jambo la dharura,” ambayo gavana anaweza kutekeleza kupitia sheria za “utendaji, mifuatano, na amri zilizoidhinishwa kisheria.” MCL 30.403(1)-(2). Vilevile, Sheria ya Mamlaka ya Dharura ya gavana ya 1945, imeeleza kwamba, baada ya kutangaza hali ya dharaura, “gavana anaweza kutoa amri zinazoeleweka, kanuni, na maagizo anayoyaona kuwa ya lazima kulinda maisha na mali au kudhibiti hali ya dharuara katika sehemu husika.” MCL 10.31(1).

Ili kupunguza kuenea kwa kirusi cha COVID-19 na kuwawekea ulinzi mkali wakazi wa Michigan walio hatarini na mfumo wa afya wa Jimbo la Michigan na miundombinu za kimsingi, ni jambo linaloeleweka na la lazima kuweka uzuiaji wa kiwango na wa muda kuhusu uingiaji wa watu katika mahospitali, makazi ya wagonjwa, na magereza ya watoto.

Amri ya Utendaji 2020-6 iliweka vizuio hivyo. Kutokana na amri hii, Amri ya Utendaji 2020-6 imeondolewa. Amri hii imetoa masharti sawa kwa kiwango kikubwa, isipokuwa mabadiliko ya kutoa ufafanuzi kuhusu kutembelea mahali hapo ambako kumezuiliwa katika sehemu ya 1, hapo chini.

Huku masharti ya sheria hii yakiwa vinafuatwa, makazi hayo, yanapaswa, kadiri iwezekanavyo, kuendeleza kuingia kwa wageni kwa kushirikiana na viongozi kwa njia ya simu au mawasiliano kupitia jukwa za kiteknolojia, kulingana na sera za kawaida za kutembelewa na wageni.

Amri ya Utendaji 2020-7 ilitoa masharti kama hayo. Amri hii inafafanua masharti hayo na kuongeza muda wa masharti hayo, kwa vile bado ni ya busara na lazima ili kuimarisha afya na usalama wa jimbo hili na wakazi wake dhidi ya ugonjwa wa Korona (COVID-19). Amri hii imeiondoa Amri ya Utendaji 2020-7.

Nikifuata Katiba ya Michigan ya 1963 na Sheria ya Michigan, ninaamrisha yafuatayo:

1. Kuanzia sasa na ikiendelea mpaka tarehe 3, mwezi wa tano (au Mei) mwaka wa 2020, saa tano na dakika hamsini na tisa usiku, mahospitali, makazi ya wagonjwa, makazi ya pamoja ya wagonjwa, na magereza ya watoto, lazima yazuie kuingia humo wageni ambao: hawahitajiki kwa utoaji wa huduma za kimatibabu, kutoa huduma muhimu za kila siku, au kutekeleza shughuli za mawakili au msimamizi aliyeteuliwa na mahakama kwa ajili ya mkazi wa hapo; sio mzazi, mzazi msimamizi, au msimamizi wa mtu aliye na umri wa miaka 21 au chini anayeishi humo; hawamtembelei mkazi anayeishi humo na asiye katika hali ya hatari au huduma za mwisho wa maisha yake; na hawako huko kwa ajili ya kutekeleza majukumu muhimu ya serikali.
2. Kuanzia hivi sasa ikiendelea hadi tarehe 3, mwezi wa tano (au Mei), mwaka wa 2020, saa tano na dakika hamsini na tisa usiku, mahospitali yote, makazi yote ya wagonjwa, makazi yote ya pamoja ya wagonjwa, na magereza yote ya watoto, lazima yapime hali ya afyya ya watu wote ambao hawaishi humo kila wanapoingia humo, na lazima wawazuie kuingia humo watu ambao hawafikii viwango vya afya vilivyowekwa. Vipimo lazima vijumlishe: dalili za maambukizi ya upumwaji, kama vile, homa, kikohozi, upungufu wa hewa ya kupumua, au kuwashwa koo; na waliotangamana katika siku 14 zilizopita na mtu aliyethibitishwa kuwa na kirusi

cha COVID-19.

3. Huku masharti ya amri hii yakifuatwa, hospital zote, makazi yote ya kuhudumia wagonjwa, makazi yote ya pamoja ya wagonjwa, na magereza yote ya watoto lazima yajibiidishe kuweka utaratibu jinsi ya kupokea wageni wanaowatembelea wakazi wao kwa njia ya simu au mawasiliano ya aina nyingine za tekinolojia kama inavyowezekana, kulingana na kaida za kupokea wageni hapo.
4. Kwa ajili ya amri hii, “makazi ya kuhudumia wagonjwa” ni pamoja na, lakini si hivi tu, makazi ya wazee, nyumbani kwa wagonjwa, makazi ya muda wa watu wazima, hospital za walio karibu kufa, hospital za wagonjwa wa madawa ya kulevya, na makazi ya waliohitaji kusaidiwa ili kuishi.
5. Kulingana na MCL 10.33 na MCL 30.405(3), mtu akikaidi sheria hii kwa hiari, atashitakiwa.
6. Amri ya Utendaji 2020-7 imeondolewa au imefutwa.

Imetolewa chini ya mkono wangu na Nembo Kuu ya Jimbo la Michigan.

Tarehe: Aprili 5, 2020
Saa: 11:36 jioni



GRETCHEN WHITMER
GOVERNOR

Na Gavana:

SECRETARY OF STATE